MMUST PUBLISHING PRESS

**Jarida la Kiswahili Sanifu**




# Tathmini ya Masuala ya Ulemavu miongoni mwa Watoto wa Shule za Msingi

Stephen M. Mwendwa[1], Pamela M.Y. Ngugi[2] Beth N. Mutugu[3]
mwendwastins@yahoo.com; ngugi.pamela@ku.ac.ke; mutugu.beth@ku.ac.ke
Chuo Kikuu cha Kenyatta

**IKISIRI**

Makala hii imetathmini upokezi wa masuala ya ulemavu miongoni mwa watoto wasomaji katika hadithi teule. Katika tasnia ya fasihi kwa jumla, tafiti zinazohusiana na masuala ya ulemavu zimefanywa. Hata hivyo, tafiti nyingi za awali zimelenga; mtindo, wahusika, msigano wa majina ya ulemavu na hata semi na lugha. Aidha, katika fasihi ya watoto, tafiti za awali zimelenga mitazamo ya watoto kwa wenzao walio na ulemavu wa kimwili pekee. Ni katika msingi huu ambapo makala hii imetathmini upokezi wa masuala ya ulemavu miongoni mwa watoto wasomaji. Ili kufikia azma hii, watafiti waliwahoji wanafunzi wa gredi ya kwanza na ya pili kutoka shule za msingi Kaunti ya Kiambu. Makala hii imeongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ya Fish (1970). Kulingana na nadharia hii, msomaji hupokea na kufasiri kazi ya fasihi kwa njia tofauti kutegemea uzoefu wake wa usomaji, maisha na hisia zake. Data iliyochambuliwa ilikusanywa maktabani na nyanjani. Maktabani mtafiti alisoma machapisho mbalimbali kama vile makala, tasnifu na vitabu vilivyolenga mada husika. Nyanjani mtafiti aliwahusisha wanafunzi wa gredi ya kwanza na ya pili kutoka shule za msingi Kaunti ya Kiambu. Matokeo ya utafiti yalibaini kwamba maoni ya watoto wasomaji haswa kutoka SK (Shule ya Kawaida) na SJ (Shule Jumuishi) yalishahabiana kwa kiwango kikubwa baada ya kusoma na kuchambua hadithi teule. Uelewa wao wa masuala ya ulemavu ulikuwa wastani na wakati mwingine wa chini. Hata hivyo, wenzao kutoka SU (Shule ya watoto walio na Ulemavu) walionekana kuwa na uelewa wa kina kuhusiana na masuala ya ulemavu kwa kuwa wanaishi na ulemavu.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
*Hadithi, Masuala ya Ulememavu, Upokezi, Watoto wa shule za msingi*

***Historia ya Makala:***
Tarehe ya Kutumwa:30April2026
Tarehe ya Kurekebishwa: 12 Julai 2026
Tarehe ya Kukubalika:1 Agosti 2026
Mtandaoni: 30 Agosti 2026

*Mwandishi Mkuu. Simu: +254720718608; *Barua Pepe* mwendwastins@yahoo.com
Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Mwendwa, S. M; Ngugi, P.M.Y; Mutugu,B.N (2026). Tathmini ya Masuala ya Ulemavu miongoni mwa watoto wa Shule za Msingi. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(2), 60-69
© 2026
Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA)

## 1. Utangulizi

Watu walio na ulemavu hutangamana na wanajamii wengine kwa namna moja au nyingine, kwa hivyo waandishi wa fasihi kwa jumla na haswa fasihi ya watoto huandika ili kuangazia uhusiano huu kwa kuweka wazi namna mahusiano haya yanavyoendelezwa. Hivyo basi, makala hii inatathmini upokezi wa watoto wasomaji kuhusu wahusika walio na ulemavu katika vitabu teule.

Kulingana na katiba ya Kenya, mtoto ni mtu au binadamu aliye na umri chini ya miaka kumi na minane (Republic of Kenya, 2010). Aidha, Wafula (2011) anasema kuwa mtoto ni aliye kati ya miaka 0-17. Hata hivyo, utafiti huu unamchukulia mtoto kama mtu aliye kati ya miaka sita hadi saba. Mtafiti aliwalenga watoto ambao wamejiunga na shule na wameanza kutangamana na wengine na pia, wanaweza kuelewa mtiririko wa hadithi. Fasihi ya watoto ni ile ambayo msingi wa kidhamira na kimaudhui huwarejelea watoto. Fasihi hii hulenga kuzungumzia ulimwengu wa watoto kwa kuwa huakisi yale ambayo mtoto anafanya, anayowaza na pia mambo yanayomkuta katika maisha yake (Bakize, 2014).

Kwa mujibu wa Katiba ya Taifa la Kenya (2010), ulemavu unaweza ukawa wa kimwili, kihisia, kiakili au ugonjwa ambao athari zake ni za kudumu na hivyo basi kumzuia mtu kutekeleza shughuli zake za kawaida za kila siku. Ulemavu ni hali ya kutokuwa na uwezo wa kutekeleza shughuli za kawaida za kila siku kama watu wengine kutokana na ulemavu wa viungo, akili au hata tabia (International Labor Organization, 2007). Vilevile, Mahenge (2017) anaeleza kuwa watu wenye ulemavu ni kama vile; walemavu wa viungo, albino, wasiosikia, wasioona, wasiokuwa na uwezo wa kuzungumza, wasiosikia-wasioona, wasiosikia-wasio na uwezo wa kuzungumza na wasiosikia, wasioona na wasio na uwezo wa kuzungumza. Isitoshe, Mutugu (2019) anasema kwamba, ulemavu ni hali inayoonesha kupungukiwa kwa namna fulani kwa mtu kutokana na namna anavyoonekana na hata tabia zake. Kutokana na fasili hizi, mlemavu ni binadamu aliye na upungufu wa kimaumbile ya kudumu.

Kulingana na Rosenblatt (1978), **upokezi ni mwingiliano kati ya msomaji na maandishi.** Rosenblatt (Keshatajwa) **anaongeza kuwa, kila msomaji huunda maana kulingana na uzoefu na hisia zake**. Aidha, Hickman (1981) ameeleza upokezi kama tabia yoyote inayodhihirisha uhusiano kati ya watoto na fasihi. Katika uchunguzi wake, aligundua kuwa watoto wa miaka 5 na 6 hupokea fasihi kupitia miondoko ya mwili kama vile; kucheza densi au hata kupiga makofi. Wakishadidia kauli hii, Martinez, Roser na Dooley (2003) wanaongeza kuwa, watoto hupokea matini kwa njia tofauti na upokezi wao hutofautiana kiumri. Karuga (2005) anahoji kuwa, upokezi ni ule mwingiliano wa papo kwa hapo kati ya msomaji na matini. Kutokana na kauli za wataalamu hawa, upokezi katika fasihi ya watoto ni mchakato wa namna watoto wanavyoelewa, kupokea, kufurahia na hata kufasiri kazi za fasihi zinazowalenga kama vile hadithi.

### 1.1 Msingi wa Nadharia

Makala hii imeongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ya Fish, (1970). Nadharia hii imeendelezwa na Iser (1974), Tompkins (1992) na Ngugi (2009). Kulingana na nadharia hii, msomaji hupokea na kufasiri kazi ya fasihi kwa njia tofauti kutegemea uzoefu wake wa usomaji, maisha na hisia zake. Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ilimfaa mtafiti kushughulikia namna masuala ya ulemavu yanavyopokelewa na watoto katika hadithi teule. Haswa mhimili unaozingatia kuwa, maarifa na tajriba aliyo nayo msomaji huathiri namna ambavyo ataifasiri matini.

### 1.2 Mbinu za Utafiti

Kwa mujibu wa Makau (2021), utafiti wa kimaelezo ni utaratibu wa kuchunguza sifa bainishi katika jambo linalofanywa na mtafiti, jinsi lilivyo na kisha kulirekodi. Muundo wa kimaelezo ulitumiwa kuchunguza upokezi wa masuala ya ulemavu miongoni mwa watoto katika shule za msingi, Kaunti ya Kiambu. Ili kufikia azma hii, kaunti ndogo tatu ziliteuliwa kimaksudi. Shule ya msingi ya Joytown Special School ilioko Thika ya watoto walio na ulemavu na Kwihota Special Unit ilioko Ruiru; shule jumuishi ziliteuliwa kimaksudi. Kulingana na Kothari (2003), asilimia thelathini ya watu inaweza kutumika kama kiwakilishi mwafaka cha sampuli ya utafiti. Kigezo hiki cha Kothari (Keshatajwa) kilitumika kuweka wazi idadi ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti. Mtafiti aliwaongoza watoto wa gredi ya kwanza na ya pili kusoma na kuchambua hadithi teule. Kwa mujibu wa Bressler (2003), ni vyema msomaji kuulizwa maswali ili kubaini upokezi wake kuhusu ulemavu. Hivyo, mtafiti aliwasaili watoto kwa kutumia kielelezo cha maswali na kisha kurekodi majibu yao kwenye tepu rekoda. Isitoshe, mtafiti alisikiliza kwa makini majibu ya wanafunzi kutoka kwa tepu rekoda. Majibu ya watoto yalimsaidia mtafiti kudondoa, kupanga na kuchanganua hoja muhimu kwa mujibu wa lengo na vigezo vya uanishaji.

## 2.0 Upokezi wa Masuala ya Ulemavu Kulingana na Wanafunzi wa Gredi ya Kwanza

Kwa mujibu wa Cochran-Smith (1984), aina za maswali na maoni ambayo watoto hutoa wakati wa mchakato wa kusoma hadithi yanaweza kutumiwa kupata ufahamu kuhusu namna watoto wanavyojenga maana na kuelewa maandishi. Mchakato huu hutufahamisha wanachokijua watoto na hata wanachotaka kujua kuhusu

maandishi. Kulingana na Mendez (2009), baada ya kusoma kazi ya fasihi, watoto huweza kuonesha upokezi na uelewa wao kwa njia tofauti kama vile: kuongea kuhusu kazi hiyo, kuandika au kutunga kisa, kuigiza na kushiriki katika shughuli zingine darasani. Kwa mintarafu hiyo basi, mtafiti aliwaongoza watoto kutoka SK, SJ na SU kusoma hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (Rajula, 2019) ili kutathmini upokezi wao kuhusu masuala ya ulemavu. Mtafiti aliwaongoza watoto kujibu kielelezo cha maswali. Baadhi ya maswali yalihusisha picha ya mhusika mwenye ulemavu, uwezo wa mhusika aliye na ulemavu, changamoto zinazomkumba mhusika aliye na ulemavu na mwisho, mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto hizi. Kwa kufanya hivi, mtafiti aliweza kubainisha upokezi wao kuhusu masuala ya ulemavu.

## 2.1 Upokezi wa Picha ya Mhusika Mwenye Ulemavu

Kwa mujibu wa Martinez, Roser na Dooley (2003), watoto huelewa zaidi picha kuliko ustadi au ubunifu wa mwandishi. Wakishadidia kauli hii, Mwendwa, Ngugi na Ndungo (2020) wanasema kuwa, matumizi mazuri ya picha katika hadithi yanaweza kuchangia kupitisha ujumbe na hivyo basi, kumfanya mtoto kuielewa hadithi. Kauli za watafiti wa awali zilimchochea mtafiti kutumia kipengele cha picha ili kubaini upokezi wa watoto kuhusu ulemavu. Watoto kutoka SK, SJ na SU walifasiri picha mbili zilizomlenga mhusika mtoto aliye na ulemavu. Tazama Tak.1 kutoka *Rafiki yangu Kilomi* (Rajula, 2019:8).



**Tak.1: Picha ya mtoto mwenye ulemavu**

Mtafiti aliwaongoza wanafunzi kutaja aina ya ulemavu unaomkumba mhusika Kilomi katika picha ya tak.1 kutoka hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (Rajula, 2019:8). Maelezo yao yalikuwa kama yafuatayo:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Ni mgurudumu. Mtu wa kuvunjika mguu. *Mwojû*. | Kilomi ameumia mguu. Kilomi ni mtoto wa Mungu. Kilomi ni *kilema*. | Hawezi kutembea. Ni mtu mwenye ulemavu wa miguu. |

Tak.2 Jedwali la maelezo ya watafitiwa kuhusu aina ya ulemavu

Jedwali katika tak.2 linaonesha maelezo ya wahusika kuhusu aina ya ulemavu. Maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU yalitofautiana haswa kuhusiana na jina faafu la mhusika aliye na ulemavu. Kwa mfano, watoto kutoka SK hawakuweza kufahamu jina faafu la mhusika aliye na ulemavu katika hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (Rajula, 2019-Uk:8). Hata ingawa watoto kutoka SJ waliweza kubaini kuwa Kilomi ni *kilema*, majibu yao mengine yalionesha kuwa uelewa wao kuhusu masuala ya ulemavu ni finyu. Kwa mfano, kudai kuwa mhusika Kilomi ameumia mguu na kuwa ni mtoto wa Mungu, ni ishara kwamba, upokezi wao kuhusu masuala ya ulemavu ni finyu. Hata hivyo, huenda maoni ya mtoto kutoka SJ yamehusishwa na imani ya dini fulani. Deuel na John (2023) wanaeleza kwamba, kila mtoto anayezaliwa ni zawadi kutoka kwa Mungu ikiwa ni pamoja na wale walio na ulemavu. Akishadidia kauli hii, Mbijima (2024) anaongeza kwamba, waumini wa dini mbalimbali huchukulia kuwa, sisi wote ni watoto wa Mungu. Vilevile, watoto kutoka SJ kutumia neno *kilema* ni ishara kwamba, wameathiriwa na mazingira wanamotoka. Kwa mujibu wa Mahenge (2017), watu wenye ulemavu wanapendelea neno *mlemavu* badala ya neno *kilema*. Hii ni kwa sababu, ngeli ya KI/VI katika Kiswahili inahusishwa na vitu visivyo na uhai ambavyo huanza na kiambishi ‘ki’ katika umoja na ‘vi’ katika wingi. Hivyo basi, kumwita mtu *kilema* ni kumdhalilisha na kumfanya ajisikie vibaya kutokana na kulinganishwa na kitu. Aidha, watu wenye ulemavu wanapendekeza kujumuishwa katika ngeli ya M/WA ambayo huhusisha viumbe hai kama vile; wanyama, wadudu na hata ndege. Watoto kutoka SU waliweza kubaini kuwa Kilomi ni mtu mwenye ulemavu wa miguu na hivyo basi, hawezi kutembea. Ni dhahiri kuwa, maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU yanatofautiana kwa mujibu wa maarifa na tajriba waliyonayo. Kwa mfano, kuna wale wameathiriwa na mazingira wanamotoka na hivyo basi kutumia neno *kilema*. Aidha, kuna wale wameathirika na lugha zao za kwanza. Mfano ni matumizi ya neno *mwojû* ambalo ni la kutoka kwa jamii ya Wagikuyu kumaanisha mlemavu. Mwisho,

athari ya imani ya dini ya Kikristo ni wazi pia. Kauli za watoto hawa zinaingiliana na mhimili wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji (Fish, 1970) unaosema kuwa, maarifa na tajriba aliyo nayo msomaji huathiri namna ambavyo ataifasiri matini teule.

## 2.2 Upokezi Kuhusu Uwezo wa Mhusika Mwenye Ulemavu

Uwezo ni sifa au ujuzi alio nao mtu wa kufanya jambo fulani. Kwa mujibu wa Blaska (2004), watoto wote wanahitaji kuwa na nafasi ya kujifunza kuhusu tofauti za uwezo wa watu wenye ulemavu kama wanavyofundishwa kuhusu tofauti za kitamaduni. Mtafiti aliwaongoza watoto kutoka SK, SJ na SU kusoma hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (Rajula, 2022) na kisha kutoa kauli zao kuhusiana na mhusika Kilomi aliyekuwa na ulemavu wa miguu. Aidha, walisema kuwa mhusika Kilomi anaweza kufanya mambo yafuatayo:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Kusoma hadithi.<br>Kuomba usaidizi.<br>Kucheza.<br>Kuimba.<br>Kuhesabu. | Kusoma.<br>Kusikiliza rafiki yake anachokisema.<br>Kucheza mpira.<br>Kuimba.<br>Kuandika.<br>Kujilisha chakula. | Kusoma.<br>Kuoga.<br>Kusukuma kiti chake cha gurudumu.<br>Kuandika.<br>Kuimba.<br>Kula.<br>Kuvalia nguo.<br>Kuosha vyombo. |

Tak.3 Jedwali la maelezo ya watafitiwa kuhusu mambo anayoweza kufanya Kilomi

Watoto kutoka SK, SJ na SU wameeleza uwezo wa mhusika Kilomi na hata watu wenye ulemavu kwa jumla kama inavyojitokeza katika jedwali la Tak.3. Blaska (2004) anasema kwamba, ni muhimu watoto kujifunza kuhusu ulemavu na magonjwa katika mtaala mzima ili wanapopata fursa ya kuungana au kuwa na wenzao wenye ulemavu darasani, wawe na ufahamu na uelewa wa awali kuhusu masuala ya ulemavu. Upokezi wa watoto kutoka SK, SJ na SU kuhusu masuala ya ulemavu unaonesha kuwa, wana uelewa kuhusu masuala ya ulemavu haswa kwa kulenga uwezo wa watu wenye ulemavu. Kwa mfano, ingawa mtoto mwenye ulemavu ana changamoto za kutembea, hana kikwazo kingine. Hili linathibitishwa na msomaji kutoka SJ anaposema kuwa, mhusika mwenye ulemavu anaweza kusikia anachokisema rafiki yake. Hii inaashiria kuwa, mtoto msomaji anafahamu kuwa kuna aina tofauti za ulemavu.

## 2.3 Upokezi wa Changamoto Zinazomkumba Mtu Mwenye Ulemavu

Watoto kutoka SK, SJ na SU walieleza changamoto zinazomkumba mtu mwenye ulemavu baada ya kusoma hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (Rajula, 2019). Aidha, walisema kwamba, mhusika Kilomi hawezi:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Kutembea.<br>Kuruka.<br>Kudensi.<br>Kucheza mpira kwa miguu.<br>Kukimbia.<br>Kusimama.<br>Kubeba rafiki yake kwa mgongo.<br>Hawezi *kubalance* akienda *kudance*. | Kutembea.<br>Kukimbia.<br>Kulala.<br>Kuchota maji mtoni.<br>Kusimama.<br>Kuosha vyombo.<br>Kuruka.<br>Kupiga mpira.<br>Kuoga.<br>Kuimba.<br>Kuinuka. | Kutembea.<br>Kukimbia.<br>Kujifulia nguo.<br>Kusimama.<br>Kuchota maji mtoni.<br>Kujivalisha nguo.<br>Kupiga mpira.<br>Kusimama.<br>Kufikia kitu |

Tak.4. Jedwali kuhusu changamoto zinazomkumba mtu mwenye ulemavu

Kulingana na watoto kutoka SK, SJ na SU, mtu mwenye ulemavu hukumbwa na changamoto nyingi kama inavyoelezwa katika jedwali la Tak.4. Hata ingawa mhusika Kilomi ana ulemavu, baadhi ya mambo ambayo watoto kutoka SJ na SU walisema kumhusu, sio ya kweli. Kwa mfano, watoto kutoka SJ walisema kuwa, mhusika Kilomi hawezi; kulala, kuosha vyombo, kuimba na kupiga mpira. Aidha, watoto kutoka SU walidai kuwa, Kilomi hawezi kujifulia na hata kujivalisha nguo. Mhusika Kilomi ana ulemavu wa miguu na hivyo basi, baadhi ya changamoto anazolimbikiziwa na watoto kutoka SJ na SU sio sahihi. Maoni ya watoto kutoka SJ na SU yanatokana na tajriba walio nayo kuhusu suala la ulemavu. Ni wazi kwamba, maoni yao yanaafikiana na yale ya Fish (1970) katika nadharia ya Mwitikio wa Msomaji haswa mhimili unaozingatia kwamba, maarifa na tajriba aliyo nayo msomaji huathiri namna atakavyoifasiri matini. Vilevile, maoni ya watoto kutoka SJ na SU yana ugiligili na yale ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloeleza kwamba, watu wasio na ulemavu hulazimika "*kutunza*" watu wenye ulemavu na mara nyingi husawiriwa kama mzigo kwa jamii, familia na marafiki (United Nations, 2014).

## 2.4 Mapendekezo ya Namna ya Kukabiliana na Changamoto zinazomkumba Mtu Mwenye Ulemavu

Baada ya kusoma hadithi ya *Rafiki yangu Kilomi* (Maina, 2022), mtafiti aliwaongoza watoto kutoka SK, SJ na SU kutoa mapendekezo yao ya jinsi ya kusuluhisha changamoto zinazomkumba mhusika Kilomi. Kauli za watoto kutoka SK na SJ kuhusu mapendekezo yao ya kutatua changamoto zinazomkumba mhusika Kilomi zinaonesha

kwamba, upokezi wao kuhusu masuala ya ulemavu ni wa kiwango cha chini kama inavyobainika katika jedwali la Tak.5 ifuatavyo:

| SK | SJ | SU |
| --- | --- | --- |
| Anafaa kunyamaza.<br>Hafai kuuliza maswali mengi.<br>Anafaa kusaidiwa na rafiki yake.<br>Anafaa kutembelea rafiki yake.<br>Anafaa kufanyiwa mazoezi na hata kusaidiwa na daktari. | Kusoma.<br>Kuandika.<br>Kutii walimu.<br>Kuheshimu wazazi wake.<br>Aende kanisani aombewe ili Mungu aponye.<br>Aende hospitali.<br>Asaidiwe na wazazi wake. | Anafaa kutumia kiti chake cha magurudumu.<br>Anafaa kufanya mazoezi. |

Tak.5. Mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto zinazomkumba Kilomi

Mathalan, maoni ya watafitiwa kutoka SK kuwa mtu mlemavu hafai kuuliza maswali mengi kama suluhisho yanaashiria kuwa anapaswa kuridhika na hali yake, anyamaze tu na kwamba watu walio na ulemavu hawana mambo mengi ya maana ya kusema, hivyo wanapaswa kunyamaza. Wakikubaliana na kauli hii, Zhang na Haller (2013) wanaongeza kwamba, vyombo vya habari vimewasawiri watu wenye ulemavu kama wagonjwa na waathiriwa wasiojiweza na wanaokumbwa na unyanyapaa kwani maisha yao husawiriwa kama yasio na thamani haswa kwa kuyalinganisha na ya watu ambao hawana ulemavu. Aidha, maoni ya watoto kutoka SJ yanaashiria kuwa, ulemavu unatokana na kutoheshimu wazazi, hivyo akiwaheshimu wazazi atapata nafuu. Maoni haya yanaingiliana na yale ya Stone-MacDonald na Butera (2012) wanaosema kwamba, imani ya jadi ilishikilia kuwa, ulemavu ni adhabu kwa matendo mabaya yanayofanywa na watu. Kadhalika, mtoto kutoka SJ kusema kuwa maombi yatamfaa mtu mwenye ulemavu ni suala linalohusu imani ya kidini katika kusuluhisha changamoto za watu wenye ulemavu ambao mara nyingi hushia kupotoshwa na imani hizi. Vivyo hivyo, Wakristo wengi wanaamini kwamba, ulemavu ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu (Stone-MacDonald na Butera, 2012). Hata hivyo, watoto kutoka SU walionesha kuwa na upokezi wa masuala ya ulemavu kwani, kauli zao ziliashiria kutatua changamoto za kutembea zinazomkumba mhusika Kilomi aliye na ulemavu wa miguu kama vile kutumia kiti cha magurudumu na hata kufanya mazoezi ya viungo.

**3.0 Upokezi wa Masuala ya Ulemavu Kulingana na Wanafunzi wa Gredi ya Pili**

Sehemu hii ya pili imetathmini upokezi wa masuala ya ulemavu kulingana na wanafunzi wa gredi ya pili katika shule teule za msingi, Kaunti ya Kiambu. Watoto kutoka SK, SJ na SU walichambua hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000) na *Mwanasesere wa Mosi* (Kitunga, 2002). Ili kutathmini upokezi wao kuhusu masuala ya ulemavu, mtafiti aliwaongoza watoto kujibu kielelezo cha maswali. Muriuki (2022) anasema kwamba, watoto wanaweza kuonesha maarifa waliyopata baada ya kusoma na kutoa maoni ya kile walichosoma. Kwa msingi huu basi, mtafiti aliwasaili watoto watafitiwa maswali yaliyohusisha picha ya mhusika mwenye ulemavu, uwezo wa mhusika aliye na ulemavu, changamoto zinazomkumba mhusika aliye na ulemavu na mwisho, mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto hizi. Kwa kufanya hivi, mtafiti aliweza kubainisha upokezi wao kuhusu masuala ya ulemavu.

### 3.1 Upokezi wa Picha ya Mhusika Mwenye Ulemavu

Kulingana na Al-Hinaai (2010), picha zinaweza kuathiri watoto kwa njia tofauti kama vile; kubadilisha hali zao, mawazo, tabia na hata fikra zao. Picha zina majukumu mengi katika vitabu vya watoto na zinaathiri watoto haswa kwa kuwachochea kuwa na upokezi tofauti. Mtafiti aliwaongoza watoto kutoka SK, SJ na SU kufasiri picha zilizo na mhusika aliye na ulemavu kwa kutaja aina ya ulemavu katika Tak.6 na Tak.7 ili kutathmini upokezi wao. Tazama Tak.6 katika hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000).



**Tak.6: Picha ya mtoto mwenye ulemavu pamoja na wazazi wake**

Mtafiti aliwaongoza watoto wa SK, SJ na SU kutaja aina ya ulemavu unaomkumba mhusika Daudi katika picha ya Tak.6 kama inavyojitokeza katika hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000:1). Walieza kuwa mhusika Daudi ni:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Mlemavu. Kiwete. | Mvulana mwenye ulemavu. | Mvulana mwenye ulemavu. Mvulana anayetembea na mkongojo na hivyo basi, ana ulemavu. |

Tak.7. Maelezo ya watafitiwa kuhusu aina ya ulemavu

Maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU yanaonesha kwamba, uelewa na upokezi wao kuhusu masuala ya ulemavu haswa kwa kutumikiza picha ni wa kiwango cha juu kwani waliweza kutambua aina ya ulemavu unaomkumba mhusika Daudi kama inavyodhihirika katika jedwali la Tak.7. Maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU yanashahabiana na yale ya Brookshire, Scharff na Moses (2002) wanaosema kwamba, kutazama picha kabla ya kusoma huwapa watoto taarifa ambazo zinaweza kuimarisha kusoma na kufasiri matini. Aidha, wanaongeza kwamba, kutazama picha baada ya kusoma huthibitisha kile kilichosomwa pamoja na kutoa taarifa zaidi kuhusu mazingira na matukio.

Vilevile, mtafiti aliwaongoza watoto wa SK, SJ na SU kuchambua picha nyingine katika hadithi ya *Mwanasesere wa Mosi* (Kitunga, 2002:12-13). Kulingana na Feathers na Arya (2012), picha hutumika kutoa habari kuhusu wahusika, kuonesha hisia zao kupitia ishara za uso na maumbile yao ya mwili. Kushiriki na kusoma vitabu vya picha mara kwa mara kunawezesha watoto kusoma mapema, na hata kufikiria mitazamo yao kwa kina wakati wa kuchambua mijadala ya kijamii (Vasquez, Janks na Comber, 2019). Zifuatazo ni fasiri za watoto kutoka SK, SJ na SU kuhusu picha katika Tak.8 kutoka *Mwanasesere wa Mosi* (Kitunga, 2002:12-13)



**Tak. 8: Picha ya watoto wenye ulemavu walipotembelewa na Mosi katika kituo cha Tumaini**

Mtafiti aliwaongoza watoto kutoka SK, SJ na SU kutaja aina ya ulemavu uliowakumba watoto katika picha ya Tak.8. Watoto kutoka SK, SJ na SU walisema kuwa waliona:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Watoto wenye ulemavu. | Watoto wenye ulemavu. | Watoto wenye ulemavu; wavulana kwa wasichana. Watoto wenye ulemavu wa kutembea. |

Tak.9 Jedwali la maelezo ya watafitiwa kuhusu aina ya ulemavu

Watoto kutoka SK, SJ na SU waliweza kubaini kuwa wahusika walio kwenye picha ya Tak.8 ni watoto walio na ulemavu kama inavyojitokeza katika jedwali la Tak.9. Tofauti na watoto kutoka SK na SJ waliotaja tu kuwa wahusika watoto wana ulemavu, watoto wa SU walitambua kuwa wahusika walio na ulemavu walikuwa na ulemavu wa miguu na pia, walikuwa wavulana na wasichana. Hata ingawa watoto kutoka SK na SJ walifasiri picha ya Tak.8 sahihi, hawakutaja aina ya ulemavu moja kwa moja kama walivyofanya watoto wa SU. Maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU yanashadidiwa na yale ya Feathers na Arya (2012) wanaosema kuwa, picha hutumika kuthibitisha kile kilichosomwa; iwe ni neno, kifungu, sentensi au ukurasa mzima. Picha ya Tak.8 iliweka wazi kile watoto wa SK, SJ na SU walifahamu kuhusu picha lengwa.

### 3.2 Upokezi Kuhusu Uwezo wa Mhusika Mwenye Ulemavu

Mtafiti aliwaongoza watoto kutoka SK, SJ na SU kusoma hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000) na kisha kuwaelekeza waeleze uwezo wa mhusika mkuu Daudi aliye na ulemavu wa mguu. Maoni ya watoto wa SK, SJ na SU yalikuwa kama ifuatavyo:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Kufundisha. Kucheza. Kuendesha basi. Kushika mwizi. Kusaidia watu. Kupika. Kufanya kazi. Kuwa mwalimu. Kuoga. | Kupika. Kutembea. Kubeba kitu. Kusaidia kama vile; kutega mwizi. Kusikia. Kuongea. Kuona. | Kujipigania. Alitega mwizi. Kushona. Kufua nguo. Kusoma. |

| | | |
|---|---|---|
| Kuchora. | | |

Tak.10 Jedwali la Maelezo ya watafitiwa kuhusu mambo anayoweza kufanya Daudi

Kulingana na watoto kutoka SK na SU mhusika aliye na ulemavu anaweza kufanya majukumu mbalimbali sawia na watu ambao hawana ulemavu wa viungo kama inavyobainika katika jedwali la Tak.10. Kauli za watoto kutoka SK na SU zinaungwa mkono na baadhi ya watoto wa SJ ambao wana maoni mseto kuhusu uwezo wa mhusika Daudi. Kuna baadhi ya watoto kutoka SJ ambao walidai kuwa mhusika Daudi anaweza; kusikia, kuongea na kuona ilhali uwezo huu nao tayari. Kauli hizi kutoka kwa watoto wa SJ zinaonesha kuwa upokezi wao kuhusu uwezo wa mtu mwenye ulemavu wa viungo ni wa chini. Aidha, msimulizi katika hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000) amethibitisha waliyosema watoto wa SJ kwa kumsawiri mhusika Daudi kama mwenye uwezo wa kusaidia jamii wakati wa hatari. Mtafiti alinuia kupata upokezi wao kuhusu uwezo wa majukumu mbalimbali ambayo Daudi anaweza kutekeleza licha ya ulemavu wake. Hivyo, ni wazi kwamba, upokezi wa masuala ya ulemavu miongoni mwa watoto kutoka SK, SJ na SU unatofautiana.

Pia, mtafiti aliwaongoza watoto kutoka SK, SJ na SU kusoma hadithi ya *Mwanasesere wa Mosi* (Kitunga, 2002) na kisha kueleza kuhusu uwezo wa wahusika watoto walioishi katika kituo cha Tumaini. Yafuatayo ni maoni ya watoto watafitiwa kuhusu uwezo wa wahusika wenye ulemavu:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Kupika.<br>Kuandika.<br>Kuchora.<br>Kusaidiana.<br>Kutengeneza vitu.<br>Kutengeneza wanasesere.<br>Kuongea.<br>Kuwa walimu.<br>Kupaka rangi. | Kutengeneza wanasesere.<br>Kusaidia watu wengine.<br>Kutega mwizi.<br>Kupika.<br>Kufua nguo. | Kutengeneza baiskeli.<br>Kutengeneza bangili.<br>Kutengeneza basi.<br>Kutengeneza wanasesere.<br>Kutengeneza gari. |

Tak.11 Jedwali la Maelezo ya watafitiwa kuhusu mambo wanayoweza kufanya watoto walio na ulemavu katika kituo cha Tumaini.

Mitazamo ya watoto kuhusu watu wenye ulemavu inaweza kuathiriwa na jinsi wahusika wenye ulemavu wanavyosawiriwa katika fasihi (Adomat, 2014; Cameron & Rutland, 2006; Smith-D'Arezzo & Moore-Thomas, 2010). Kwa mfano, katika hadithi ya *Mwanasesere wa Mosi* watoto wahusika walio na ulemavu wamesawiriwa kama wenye uwezo wa kutekeleza majukumu mbalimbali. Aidha, hili linasisitizwa na maoni ya watoto kutoka SK, SJ na SU kwamba, watu wenye ulemavu wana uwezo wa kufanya mambo mbalimbali kama inavyodhihirika katika jedwali la Tak.11. Wahusika wenye ulemavu katika hadithi ya *Mwanasesere wa Mosi* (Kitunga, 2002) wamesawiriwa na kukuzwa kama binadamu wa kawaida licha ya kuwa na maumbile tofauti. Upokezi wa masuala ya ulemavu miongoni mwa watoto kutoka SK, SJ na SU ni wa juu haswa baada ya kusoma hadithi ya *Mwanasesere wa Mosi* (2002) kwani waliweza kueleza kuwa mtu aliye na ulemavu ana uwezo wa kufanya vitu vingi kama vile kuchora, kusaidia watu wengine, kutengeneza vitu mbalimbali miongoni mwa vitu vingine.

### 3.3 Upokezi wa Changamoto Zinazomkumba Mtu Mwenye Ulemavu

Baada ya kusoma hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000), mtafiti aliwaongoza watoto kutoka SK, SJ na SU kutaja changamoto zinazomkumba mhusika Daudi aliye na ulemavu wa miguu. Kulingana na watoto watafitiwa changamoto zinazomkumba Daudi ni kama vile:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Kutembea.<br>Kuongea.<br>Kuruka.<br>Kuoga.<br>Kujipatia chakula.<br>Kucheza vizuri.<br>Kuona/kusikia. | Kufua nguo.<br>Kukimbia.<br>Kutembea.<br>Kucheza.<br>Kupigana.<br>Kuona/kusikia. | Watu wenye ulemavu hawakumbwi na changamoto za kipekee wao ni kama watu wa kawaida. |

Tak.12 Jedwali la Changamoto zinazomkumba mtu mwenye ulemavu

Watoto kutoka SK na SJ walikubaliana pakubwa haswa kuhusiana na changamoto zinazomkumba mhusika Daudi aliye na ulemavu wa mguu kama inavyobainika katika jedwali la Tak.12. Hata hivyo, baadhi ya changamoto zilizotajwa na watoto wa SK na SJ sio sahihi kama vile; kuongea, kujipatia

chakula, kuona, kusikia na kufua nguo. Hii ni kwa sababu, Daudi ana ulemavu wa miguu pekee. Maoni ya watoto kutoka SK na SJ ni ishara kwamba, upokezi wao wa masuala ya ulemavu ni wa chini kwani wanafikiri kuwa, ulemavu wa aina moja ni kizuizi cha kufanya vitu vingi. Kulingana na Nikolaraizi, Kumar, Favazza, Sideridis, Koulousiou na Riall (2005), mitazamo hasi mara nyingi hutokana na dhana potofu miongoni mwa watoto haswa wenzao walio na ulemavu. Aidha, wanatoa mfano kwamba, watoto wa miaka 5–7 hueleza wasiwasi kuhusu wenzao wenye ulemavu kwamba; watahitaji matibabu, kuwa na magonjwa ya kuambukiza, au hata kukosa uwezo wa kucheza.

Ni wazi kwamba, watoto kutoka SK na SJ wana upokezi wa masuala ya ulemavu kwa kiwango fulani kwani baadhi ya changamoto walizotaja kwa hakika, zinaweza mkumba mhusika Daudi na hata mtu yeyote mwenye ulemavu wa miguu. Hata hivyo, kulingana na watoto wa SU hakuna kitu ambacho kinaweza kumzuia Daudi kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Mwishowe, watoto kutoka SK, SJ na SU walisoma hadithi ya *Mwanasesere wa Mosi* (Kitunga, 2002) watoto wa SK, SJ na SU na kisha kueleza kuwa, watoto wenye ulemavu katika kituo cha Tumaini hawawezi;

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Kutembea. Kusikia. Kubeba jiwe. Kupika. Kujenga nyumba. Kuogelea. Kuruka. | Kupigana. Kurusha mawe. Kupika chakula. Kukimbia. Kucheza. Kutembea. Kuruka. | Hawana changamoto ni kama binadamu wengine ambao ni wa kawaida. |

Tak.13 Jedwali la Changamoto zinazomkumba mtu mwenye ulemavu

Changamoto zilizotajwa na watoto kutoka SK na SJ zinashahabiana kwa kiwango kikubwa kama inavyojitokeza katika jedwali la Tak.13. Hata hivyo, baadhi ya changamoto zilizotajwa na watoto wa SK na SJ sio sahihi. Kwa mfano, kusema kwamba watoto wenye ulemavu wa viungo vya mwili na hata wengine wanaotembea kwa kuchechemea hawawezi kusikia na hata kupika chakula sio sahihi. Vilevile, upokezi wa masuala ya ulemavu baina ya watoto wa SU na wenzao kutoka SK na SJ unatofautiana. Kulingana na watoto wa SU, ulemavu hauwezi kumzuia mtu kufanya anachotaka. Aidha, waliongeza kuwa ingawaje wana ulemavu, hawajashindwa kufanya wanachotaka. Matokeo haya yanaafikiana na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji yake Fish (1970) anayeeleza kwamba, upokezi wa watoto hutofautiana kulingana na kulelewa kwao, maarifa yao ya kimsingi, jinsia, dini na hata hisia zao.

**3.4 Mapendekezo ya Namna ya Kukabiliana na Changamoto zinazomkumba Mtu Mwenye Ulemavu**

Baada ya kusoma hadithi ya *Daudi Mlemavu* (Jefwa, 2000), watoto kutoka SK, SJ na SU walipendekeza suluhu kwa changamoto zinazomkumbuka mhusika Daudi. Hodkinson (2007) na Varenne (2018) wanakubaliana kwamba, tamaduni mbalimbali huwawezesha watoto kueleza wanachoweza au wasichoweza watu wenye ulemavu haswa kupitia maingiliano yao ya kila siku na wenzao, watu wazima na hata vyombo vya habari. Hata hivyo, watoto kutoka SK, SJ na SU walitoa mapendekezo yao ya suluhu kwa changamoto zinazomkumba mtu mwenye ulemavu. Walipendekeza ifuatavyo:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Aende hospitali. Aende kanisani. Asiogope. Asikasirike. Aende nyumbani. Aende kwa duka. Aache kutetemeka. | Kusaidiwa na watu wengine ambao hawana ulemavu. Apelekwe hospitali. Asipigwe. Asichokozwe/Asisumbuliwe/Asisukumwe. | Atumie kiti cha magurudumu au hata mkongojo wake wa kutembelea. Kujichunga. Afanye mazoezi ya viungo vya mwili. Afanyiwe tibamaungo. Afanye kazi akiwa ameka a chini. |

Tak.14 Jedwali la Mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto zinazomkumba Daudi

Suluhu zilizotolewa na watoto wa SK, SJ na SU zilionesha upokezi wao kuhusiana na ulemavu kama inavyobainika katika Tak.14. Kauli za watoto

kutoka SK na SJ zinaonesha kwamba upokezi wao wa masuala ya ulemavu ni wa kiwango cha chini. Kwa mfano, wanapopendekeza kuwa mhusika Daudi aliye na ulemavu wa miguu aende; kanisani, dukani na hata asiogope, asikasirike na hata asitetemeke ni dhihirisho kwamba, upokezi wao wa masuala ya ulemavu ni wa chini. Hata hivyo, kuna baadhi ya watoto kutoka SK na SJ waliopendekeza kwamba, Daudi anaweza kusaidiwa na wenzake ambao hawana ulemavu na pia, anaweza kupata usaidizi hospitali. Watoto kutoka SU walionesha uelewa wa kina haswa kwa kulenga suluhu walizopendekeza kwa mhusika Daudi kama vile; tibamaungo, mazoezi ya viungo vya mwili mara kwa mara na hata kutumia kiti cha magurudumu kutoka sehemu moja hadi nyingine. Watoto kutoka SU walikuwa na uelewa wa kina kuhusiana na suluhu kwani huo ndio uhalisia wao. Kauli hizi zinashahabiana na maoni ya Fish (1970) ambaye anasema kuwa, upokezi wa watoto hutegemea kulelewa kwao, maarifa yao ya kimsingi, dini na hata jinsia zao. Suluhu zilizotolewa na watoto kutoka SU zilidhihirisha kwamba, wana uelewa wa masuala ya ulemavu.
Isitoshe, mtafiti aliwaongoza watoto kutoka SK, SJ, SU kusoma hadithi ya *Mwanasesere wa Mosi* (Kitunga, 2002) na kisha kutoa maoni yao kuhusu watoto walioishi katika kituo cha Tumaini na walikuwa na ulemavu. Maoni ya watoto watafitiwa yalikuwa kama ifuatavyo:

| SK | SJ | SU |
|---|---|---|
| Waombe Mungu. Waende kanisani kwa lengo la kuombewa. Waende hospitali. | Wapelekwe hospitali. Wadungwe sindano, apewe dawa, atibiwe. Wasaidiwe na wengine ambao hawana ulemavu. | Wanafaa kusukumwa kwenye kiti chake cha magurudumu. Wanafaa kufanya mazoezi. Wanafaa kufanyiwa tibamaungo kila mara. Kusoma kwa bidi ili baadaye ajisaidie. Kuoga. |

Tak.15 Jedwali la Mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakumba watoto walio na ulemavu katika kituo cha Tumaini.

Watoto kutoka SK na SJ walikubaliana kwani walipendekeza kwamba, wahusika wenye ulemavu wanastahili kujishughulisha na dini na hata kwenda hospitali kama inavyodhihirika katika jedwali la Tak.15. Kulingana nao, vipengele vya dini na matibabu vitachangia kutatua changamoto zinazotokana na ulemavu. Ni wazi kuwa, watoto wa SK na SJ wanadhani kuwa mtu mwenye ulemavu ni mgonjwa na ndio maana wanapendekeza aende hospitalini. Tofauti na wenzao, watoto kutoka SU wanaonekana kupendekeza suluhu halisia kama vile kufanya mazoezi ya viungo vya mwili, kufanyiwa mazoezi ya tibamaungo kila mara na hata kutumia kiti cha magurudumu ili kurahisisha mwendo wa kutoka sehemu moja hadi nyingine. Hata hivyo, kuna baadhi ya watoto wa SU walioonesha upokezi wa kiwango cha chini kwa kudai kuwa wahusika walio na ulemavu wanastahili kuoga kama njia mojawapo wa suluhu ya changamoto zinazowakuwamba watoto walio na ulemavu.

## 4.0 Hitimisho

Makala hii imetathmini upokezi wa masuala ya ulemavu miongoni mwa watoto wa gredi ya kwanza na ya pili katika shule za msingi, Kaunti ya Kiambu. Aidha, shule teule zilisoma na kuchambua hadithi teule. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa upokezi wao ulitofautiana. Mathalan, watoto kutoka SU walionesha uelewa wa kina kuhusiana na suala la ulemavu huku wenzao kutoka SK na SJ wakionesha uelewa wastani na wakati mwingine finyu.
Kutokana na utafiti huu, imebainika kwamba watoto wanaosoma shule za kawaida wana uelewa finyu na wakati mwingine wastani kuhusu masuala ya ulemavu. Kwa hivyo, matokeo ya utafiti huu yanaweza kuwafaa wanajamii haswa wadau mbalimbali katika tasnia ya elimu. Kwa mfano, kujumuisha watoto wote kwa pamoja kutachangia kuondoa unyanyapaa dhidi ya watoto walio na ulemavu. Pia, watoto ambao hawana ulemavu watakuwa na ubinadamu zaidi kwani wataingiliana na hata kuelewa wenzao walio na ulemavu kwa kina.

**Marejeleo**

Adomat, D. S. (2014). Exploring issues of disability in children's literature discussions. In, *Disability Studies Quarterly*, *34*(3). Kur. 1-17.
Al-Hinaai, S. N. (2010). “What is the Importance and Impact of Illustrations in Children's Books?” An investigation into children's responses to illustrations. In, *Arab Journal for Scientific Publishing (AJSP)*. Kur. 2663-5798.
Bakize, L.H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing press.
**Blaska, J. (2004).** Children's literature that includes characters with disabilities or

illnesses. *Disability Studies Quarterly, 24*(1). https://doi.org/10.18061/dsq.v24i1.859. Retrieved on 03/02/2025.

Bressler, E. C. (2003). *Literary Criticism: An Introduction to Theory and Practice*. New Jersey: Prentice Hall.

Brookshire, J., Scharff, L., & Moses, L. (2002). The influence of illustrations on children's book preferences and comprehension. *Reading Psychology, 23*(4). Kur. 323-339.

Cameron, L., & Rutland, A. (2006). Extended contact through story reading in school: Reducing children's prejudice toward the disabled. *Journal of Social Issues*, *62*(3). Kur. 469-488.

Cochran-Smith, M. (1984). *The making of a reader*. Nor wood, NJ: Ablex.

Deuel, D., & John, N. G. (2023). Kings and queens on mission: The image of God in God's plan for disability. *Christian Journal of Global Health*, *10*(2). Kur. 74-79.

Feathers, K. M., & Arya, P. (2012). The role of illustrations during children's reading. *Journal of Children's Literature*, *38*(1). Kur. 36-43.

Fish, S. (1970). Literature in the Reader: Affective Stylistics. In, *New literary history*, 2(1). Kur. 123-162.

Hickman, J. (1981). A new perspective on response to literature: Research in an elementary school setting. In, *Research in the Teaching of English*, Kur. 343-354.

Hodkinson, A. (2017). Constructing impairment and disability in school reading schemes. *Education 3-13*, *45*(5). Kur. 572-585.

International Labour Organization. (2007). *The employment situation of people with disabilities: Towards improved statistical information*. Geneva, Switzerland: ILO.

Iser, W. (1974). *The Implied Reader*. Baltimore: John Hopkins.

Jefwa, J. (2000). *Daudi Mlemavu*. Nairobi: EAEP.

Karuga, M. N. (2005). Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kitunga, D. (2002). *Mwanasesere wa Mosi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Kothari, C. R. (2003). *Research Methodology*. New Delhi: New Age International Limited Publishers.

Maina, D. (2022). *Tupendane Sote*. Nairobi: Spotlight Publishers.

Mahenge, E. G. (2017). Msigano wa Majina ya Walemavu katika Jamii ya Wazungumzaji Kiswahili: Mfano kutoka Tanzania. *Kioo cha Lugha*, 11(1). Kur. 78-87. UDSM.

Makau, S. L. (2021). Uchanganuzi wa Uwiano wa Picha na Matini katika Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Kaunti ya Kakamega, Kenya. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Martinez, M., Roser, N., & Dooley, C. (2003). Young children's literary meaning making. In N. Hall, J. Larson, & J. Marsh (Eds.), *Handbook of early childhood literacy* (Kur. 222–234). London: Sage.

Mbijima, R. J. (2024). Uhakiki wa Kimwingiliano matini katika fasihi ya watoto: mambo ya msingi ya kuzingatia. *Mulika Journal*, *43*(1). Kur.136-154. https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.8. Retrieved on 03/02/2025.

Mendez, H. T. (2009). *Understanding children's response to literature* (ENGL3440). [Unpublished course module]. Chuo Kikuu cha Universida de Nova, Lisbon.

Muriuki, E. W. (2022). Tathmini ya Viwango Vya Maarifa ya Fasihi katika Shule za Msingi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mutugu, B. N. (2019). Taswira za Ulemavu kama Mtindo katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mwendwa, S. M., Ngugi, P. M., & Ndungo, C. (2020). Usilimishaji wa Vielelezo katika Fasihi ya Watoto: Mfano kutoka *Wasifu wa Mwana Kupona* (2008) na *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (2015). *Kioo cha Lugha*, *18*(1). Kur. 114-129.

Ngugi, P. M. (2009). Language and Literary Education: The State of Children's Literature in Kiswahili in Primary Schools in Kenya. Tasnifu ya Ph.D. Thesis. Chuo Kikuu Cha Vienna. (Haijachapishwa).

Nikolaraizi, M., Kumar, P., Favazza, P., Sideridis, G., Koulousiou, D., & Riall, A. (2005). A cross cultural examination of typically developing children's attitudes toward individuals with special needs. In, *International Journal of Disability, Development and Education*, *52*(2). Kur. 101-119.

Rajula, T. (2019). *Rafiki yangu Kilomi*. Nairobi: no Boundaries Ltd.

Republic of Kenya. (2010). *The Constitution*. Nairobi: Government Printers.

Rosenblatt, L. M. (1978). *The reader, the text, the poem: The transactional theory of the*

*literary work*. Carbondale, IL: Southern Illinois University Press.

Stone-MacDonald, A., & Butera, G. D. (2012). Cultural beliefs and attitudes about disability in East Africa. *Review of Disability Studies: An International Journal*, *8*(1).

Smith-D'Arezzo, W. M., & Moore-Thomas, C. (2010). Children's Perceptions of Peers with Disabilities. In, *Teaching exceptional children plus*, *6*(3). Kur. 3.

Tompkins, J. (1992). The Reader in history: The changing shape of literary response. In, *Reader Response Criticism. From Formalism to Post-Structuralism*. Kur. 201-232.

United Nations (2014). *The Convention on the Rights of Persons with Disabilities*. Training Guide. Professional Training Series No. 19. United Nations High Commissioner for Human Rights..

Varenne, H. (2018). *Successful Failure: the School America Builds*. America: Routledge.

Vasquez, V. M., Janks, H., & Comber, B. (2019). Critical literacy as a way of being and doing. In *Language arts*, *96*(5). Kur. 300-311.

Wafula, M. N. (2011, January). 'Tradition 'Versus' Modernity': Generational Conflict in *Vuta N'kuvute*, *Kufa Kuzikana*, *Msimu wa Vipepeo* and *Tumaini*. In *Swahili Forum* (Vol. 18).

Zhang, L., & Haller, B. (2013). Consuming image: How mass media impact the identity of people with disabilities. *Communication Quarterly*, *61*(3). Kur. 319-334.